

Jarida la _____ Toleo Na. 10
SAMIA TENA
10/09/2025 2025-2030



ASANTE

IRAMBA

IGUNGA

NZEGA





RAIS SAMIA: TUTAKAMILISHA UJENZI WA SKIMU KUBWA YA UMWAGILIAJI IRAMBA MASHARIKI

Mgombea urais kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dkt. Samia Suluhu Hassan, amesema akipewa ridhaa ya kuongoza tena atakamilisha skimu kubwa ya umwagiliaji iliyopo kijiji cha Ishishi kata ya Msingi yenye thamani ya bilioni 34.

Rais Samia ameyasema hayo leo Iramba Mkoani Singida wakati akihutubia maelfu ya wafuasi wa chama hicho waliofika kumsikiliza akinadi sera za chama chake.

“Lengo la mradi huu ni kuwasaidia wakulima kuvuna mara mbili kwa mwaka badala ya moja ya hapo awali”, Dkt. Samia amesema.

Skimu hii ya umwagiliaji itaongeza tija katika uzalishaji wa mazao na kuongeza kipato cha wananchi wa Iramba.





DKT SAMIA: TUTAKAMILISHA MRADI WA BILIONI 80 WA UMEME WA UPEPO MKOANI SINGIDA

Mgombea urais kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan amesema iwapo atapewa ridhaa ya kuongoza tena atahakikisha mradi wa umeme wa upepo unakamilika mkoani Singida.

Dkt. Samia ameyasema hayo leo Iramba mkoani Singida wakati akihutubia maelfu ya wafuasi wa chama hicho waliofika kumsikiliza.

“Tunaendelea kutafuta mbia wa kushirikiana naye na tumefikia hatua nzuri. Lengo ni kuondokana na nishati chafu inayotumia dizeli nk,” amesema Dkt. samia.





DKT SAMIA: VIJANA CHANGAMKIENI FURSA ZA UWEKEZAJI ZINAZOTEKELEZWA MKOANI SINGIDA

Mgombea urais kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, amewaasa vijana wa mkoa wa Singida kuchangamkia fursa za Bomba la Mafuta kutoka Hoima Uganda na mradi wa Utafiti wa gesi na mafuta unaotekelezwa katika kitalu cha Eyasi- Wembele.

Dkt. Samia ameyasema hayo leo Iramba mkoani Singida alipokuwa ananadi sera za chama chake mbele ya wananchi.

“Vijana changamkieni fursa za hiyo miradi msilale. Hizi ni fursa muhimu sana zinazopita na kufanyika mkoa huu”, amesema Dkt. Samia.



DKT SAMIA: TUNAKAMILISHA UTAFITI WA UTAFAUJI GESI NA MAFUTA EYASI- WEMBELE MKOANI SINGIDA



Mgombea urais kupitia Chama Cha Mapinduzi(CCM), Dkt Samia Suluhu Hassan amesema akipata ridhaa ya kuongoza tena atahakikisha mradi wa utafutaji gesi na mafuta wa Eyasi-Wembele mkoani Singida unakamilika.

Rais Samia ameyasema hayo leo Iramba wakati akihutubia wananchi waliofurika kumsikiliza akinadi sera za chama chake

“Mradi huu ni muhimu sana ukikamilika si tu utakuwa chachu ya maendeleo nchini bali utachochea ajira nyingi katika mkoa huu,” amesema Dkt. Samia





DKT SAMIA KUJENGA KITUO CHA KUPOKEA NA KUPOZA UMEME IGUNGA, TABORA

Mgombea urais kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM) Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan amesema akipata ridhaa ya kuongoza tena atajenga kituo cha kupokea na kupoza umeme Igunga, Tabora.

Ameyasema haya leo Igunga wakati akihutubia wafuasi waliofurika kumsikiliza akinadi sera za chama chake.

“Igunga inahitaji umeme wa uhakika ili kuhudumia kongani zitakazoanzishwa wilayani humu”, amesema Dkt Samia.

Kituo hiki kitafanya kuwa na upatikanaji wa umeme wa uhakika na kuchochea shughuli za kiuchumi Igunga.





RAIS SAMIA: TUTAJENGA SOKO KUU IGUNGA

Mgombea urais kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan amesema iwapo atapewa ridhaa ya kuongoza tena atajenga soko kuu wilayani Igunga, Tabora.

Ameyasema hayo leo wakati alipokuwa anahutubia maelfu ya wana CCM waliofurika kwa wingi kumsikiliza akinadi sera za Chama Chake.

“Ujenzi wa soko kuu katika wilaya utafungua fursa za biashara hivyo naomba ridhaa yenu ili nifanye haya”, amesema Dkt. Samia





Mgombea mwenza nafasi ya Urais kwa tiketi ya CCM Balozi Dkt. Emmanuel Nchimbi akizungumza na wakazi wa Mlele kueleza miradi mbalimbali ya maendeleo kutoka kwenye Ilani itakayowanufaisha endapo Dkt. Samia Suluhu Hassan atapewa ridhaa ya kuongoza Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.





RAIS SAMIA KUJENGA STAND MPYA YA MABASI IGUNGA, TABORA

Mgombea urais kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan amesema iwapo atapewa ridhaa ya kuongoza kipindi kingine atajenga stendi ya kisasa wilaya ya Igunga, Tabora.

Rais Samia ameyasema hayo leo wilayani Igunga alipokuwa anahutubia maelfu ya wafuasi wa chama hicho waliofurika kumsikiliza akinadi sera za chama chake.

“Mkinipa ridhaa ya kuongoza tena nitajenga stendi ya mabasi ya hadhi yake hapa Igunga,” Rais Samia amesema.





DKT. NCHIMBI: TUTAJENGA VITUO VYA AFYA, ZAHANATI NSIMBO, KATAVI

Mgombea Mwenza wa kiti cha Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dkt. Emmanuel Nchimbi, amesema kuwa iwapo chama hicho kitapata ridhaa ya kuongoza tena katika kipindi cha miaka mitano ijayo, serikali yake itajenga vituo viwili vya afya na zahanati tatu katika jimbo la Nsimbo mkoani Rukwa.

Dkt. Nchimbi amesema hayo leo alipowasili katika jimbo la Nsimbo akinadi Sera za CCM, na kumnadi mgombea Urais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, wagombea ubunge na madiwani.

"Iwapo tutapewa ridhaa ya kuongoza katika kipindi cha pili, niwahakikishie tutajenga vituo viwili vya afya na zahanati tatu ili kusogeza karibu huduma za afya kwa wananchi wa eneo hili," Dkt. Nchimbi amesema.



RAIS SAMIA KUJENGA MACHINJIO MANNE NA MAJOSHO SITA NZEGA- TABORA

Mgombea urais kupitia Chama Cha Mapinduzi(CCM), Rais Dkt.Samia Suluhu Hassan amesema akipata ridhaa ya kuongoza kipindi kingine atajenga machinjio manne na majosho sita wilayani Nzega Tabora.

Rais Samia ameyasema hayo leo wilayani Nzega wakati akihutubia maelfu ya wananchi walikusanyika kumsikiliza akinadi sera za chama chake.

“Lengo kubwa ni kuwa na nyama inayokidhi viwango vya kimataifa na mifugo yenye afya,” amesema Rais Samia.

Hili litachochea ufugaji wa kisasa na wenye tija na kuwanufaisha wafugaji.



RAIS SAMIA KUJENGA BARABARA YA PUGE-ZIBA-CHOMA(NZEGA)KWA KIWANGO CHA LAMI

Mgombea urais kupitia Chama Cha Mapinduzi(CCM), Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan amesema iwapo akipata ridhaa ya kuongoza tena atajenga barabara ya Puge, Ziba, Choma wilayani Nzega kwa kiwango cha lami.

Rais Samia amesema hayo leo wilayani Nzega wakati akihutubia maelfu ya wafuasi wa chama hicho waliofika kumsikiliza akiomba ridhaa ya kuchaguliwa kipindi kingine.

“Lengo ni kuhakikisha maeneo haya yanapitika kipindi chote cha mwaka na wananchi wanafanya shughuli zao za biashara vizuri”. Amesema Dkt. Samia.

Sambamba na hilo Rais Samia atajenga pia kwa kiwango cha lami kutoka Nzega- Itobo- Bukene kwa kiwango cha lami akipewa ridhaa ya kuongoza tena.





KONA YA ILANI

Kuendelea kudumisha
amani, utulivu na
usalama.



RAIS SAMIA KUONGEZA KILOMETA 10 NDANI YA WILAYA YA NZEGA-TABORA

Mgombea urais kupitia Chama cha Mapinduzi (CCM), Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan amesema ataongeza kilomita 10 za lami katika wilaya ya Nzega-Tabora.

Rais Samia ameyasema hayo wakati akihutubia maelfu ya wananchi leo waliokusanyika kumsikiliza akiomba ridhaa ya kuchaguliwa tena.

“Soko kuu litaendana na kilometa 10 za lami ndani ya Nzega,” amesema Rais Samia.





RAIS SAMIA AMTUA NDOO MAMA NZEGA

Mgombea ubunge wa jimbo la Nzega mjini kupitia Chama Cha Mapinduzi(CCM), Mhe. Mohamed Bashe, amesema Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ametekeleza kwa kumaliza kero ya maji Nzega.

Mhe. Bashe amesema hayo leo wilayani Nzega wakati akihutubia maelfu ya wafuasi wa chama hicho waliofika kumsikiliza Mhe. Samia akiomba ridhaa ya kuchaguliwa kipindi kingine.

“Miaka mitano iliyopita tulikuwa tukinunua dumu la maji kati ya shilingi 500 mpaka 1,000 Nzega Mjini na ili kupata maji safi na salama ilitulazimu kutembea umbali wa km 5. Ila tunakushukuru umemtua mama ndoo kichwani kwa kuwa kata 10, vijiji 21, na vitongoji vyote 176 vinapata maji safi,” Mhe. Bashe amesema.

Amesema miaka mitano iliyopita madumu 50 ya maji yalikuwa yakinunuliwa kwa shilingi 25,000 lakini sasa yana nunuliwa kwa shilingi 1,500, nakuongeza kuwa hii ndio maana ya maendeleo.



DKT. NCHEMBA: UADILIFU WA RAIS SAMIA MTAJI WA USHINDI

Mgombea ubunge kupitia Chama cha Mapinduzi jimbo la Iramba Magharibi, Dkt. Mwigulu Nchemba, amesema uadilifu alioonesha Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tangu aingie madarakani ndio mtaji unaoenda kumpatia ushindi wa kishindo kwenye Uchaguzi Mkuu Oktoba 29, 2025.

Amesema hayo leo wakati akihutubia wananchi wa wilaya ya Iramba mkoa wa Singida katika kampeni za urais.

“Mhe. Rais umeongeza makusanyo ya Serikali toka shilingi trilioni 1.2 mpaka trilioni 3, huo ni uadilifu wa makusanyo ya Serikali, lakini pia umeongeza miradi na huu ni uadilifu wa uongozi kwa kuonesha namna fedha zinavyotumika vyema kwa kubadilisha maisha ya watu,” Dkt. Nchemba amesema.





KISHOA AMSHUKURU RAIS SAMIA KWA KUTEKELEZA MIRADI MANYONI

Mgombea ubunge kupitia Chama cha Mapinduzi jimbo la Iramba Mashariki, Mhe. Jesca Kishoa, amemshukuru Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kutekeleza ilani ya chama kwa kufanya mambo makubwa katika wilaya ya Manyoni ikiwemo afya, elimu na miundombinu.

Amesema hayo leo wakati akihutubia wananchi wa wilaya ya Iramba mkoa wa Singida katika kampeni za urais nakuongeza kuwa kwa kipindi cha miaka minne dunia imejua kuwa yuko mwanamke jasiri na tunakuahidi kukuamini na kukupambania.

“Mhe Rais umefanya makubwa katika wilaya yetu ambayo ni pamoja na kutoa shilingi bilioni 8.9 kwa ajili ya marekebisho na kujenga vituo vya afya, pia kwenye elimu umetoa milioni 142 zilizo jenga madarasa na miundombinu, na kwenye upande wa barabara zimetolewa bilioni 5 ambazo zimefungua barabara mbalimbali na kiasi cha shilingi bilioni 11 zikajenga daraja kata ya Msingi ambalo ulilizindua wewe,” Mhe. Kishoa amesema.



KTOBA



KUFAKILI



*Kazi na Utu
Tunasonga Mbele*

ssh_anatekeleza